



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

ZOEZI LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA
LAANZA RASMI KATIKA MIKOA YA TANGA NA MOROGORO

Morogoro: 23 Januari, 2020

Zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura linalojumuisha mikoa ya Tanga na Morogoro (Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga na Malinyi) limeanza rasmi leo tarehe 23 Januari 2020. Zoezi hili litaendelea kwa siku saba (7) hadi tarehe 29 Januari 2020.

Uboreshaji huu unawahusu Raia wa Tanzania ambao wametimiza umri wa miaka 18 na wale ambao watatimiza umri wa miaka 18 siku ya Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba (2020). Pia, unawahusu wale ambao wamehama kutoka maeneo yao ya awali na kuhamia maeneo mengine ya Uchaguzi na wale ambao Kadi zao zimeharibika au kupotea. Zoezi la uboreshaji litahusisha kuondolewa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wale waliofariki na wengine waliopoteza sifa.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 74 (6) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ina jukumu la kuandikisha Wapiga Kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara. Hivi sasa, Tume inatekeleza zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ikiwa ni maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Hadi hivi sasa, zoezi hili limekamailika kwenye mikoa 25 ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

“Kadi yako, Kura yako. Nenda Kajiandikishe”

Imetolewa na:

Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura